# HOTUBA YA MHE. UMMY ALLY MWALIMU (MB), NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO KWENYE MAADHIMISHO YA SIKU YA KIMATAIFA YA MTOTO WA KIKE NA UZINDUZI WA KAMPENI YA "BECAUSE I AM A GIRL" (BIAAG), KARIMJEE HALL, DSM, TAREHE 11 OCT. 2012

***Watendaji wa Serikali***
***Waheshimiwa Mabalozi,***
***Wawakilishi wa Umoja wa Mataifa,***
***Wawakilishi wa Asasi za kitaifa na kimataifa,***
***Waandishi wa habari,***
***Watoto wetu wapendwa***
***Wageni waalikwa,***
***Mabibi na Mabwana.***

**Habari za Asubuhi!**
Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kuwezesha kukutana hapa kuadhimisha **Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike** ambayo inaadhimishwa tarehe 11 Oktoba ya kila mwaka. Pia siku ya leo tunashuhudia uzinduzi wa Kampeni ya "Because I am a Girl" itakayo tekelezwa hapa nchini kwetu na Plan International.

Kipekee nitoe shukrani zangu za dhati kwa Uongozi na Wafanyakazi wa Plan International kwa maandalizi ya hafla hii na kwa kunipa fursa ya kushiriki kama mgeni rasmi. Kwa niaba ya Serikali, napenda pia kuwashukuru na kuwapongeza kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wa haki, maendeleo na ustawi wa mtoto wa kike hapa nchini.

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;** Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa kike ilipitishwa rasmi na Umoja wa Mataifa mwezi Disemba mwaka 2011 na leo hii ni mara ya kwanza kuadhimishwa duniani kote. Lengo la siku hii ni kuielimisha na kuihamisisha jamii kutambua

umuhimu wa kuzingatia haki za Mtoto wa kike na kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazomkabili.

Kauli mbiu ya mwaka huu 2012 ni "***Maisha yangu, Haki yangu, Tokomeza ndoa za utotoni" (My life, My Rights, End Child Marriage)***. Kauli mbiu hii inatutaka kuwawezesha na kuwaunganisha watoto wa kike katika fursa mbalimbali ili kuwaepusha na mimba za Utotoni. Ni vyema sasa kauli mbiu hii itekelezwe kwa vitendo kwa kumwezesha mtoto wa kike kujitambua kuwa yeye ni mtu muhimu katika ujenzi wa Taifa hili.

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;** Kwa kuzingatia kauli mbiu ya mwaka huu, ningependa kutumia hadhara hii, kuongelea jitihada za Serikali katika kumpatia mtoto wa kike haki zake za msingi ikiwemo kumuepusha na mimba za Utotoni.

Moja ya hatua muhimu na kubwa nitakayoiongelea siku ya leo, ni **Kuwekeza katika Elimu ya Mtoto wa kike.** Ni ukweli usiopingika kuwa elimu ya watoto wa kike ni moja ya njia bora za kupunguza umaskini katika mataifa yanayostawi. Manufaa ya elimu yao yanaweza kuonekana kwa watu binafsi, familia zao na kwa jamii yote. Elimu ya wasichana imeonyesha kuwa na faida kubwa katika kuchelewesha ndoa na ujauzito kwa wasichana wadogo. Uzoefu unaonyesha kuwa kila mwaka wa kuelimika humsaidia msichana kufanya maamuzi bora, yake na ya familia yake. Elimu kwa wasichana ni ya kustaajabisha: Benki ya Dunia ilibainisha ya kwamba kila mwaka wa elimu huzuia vifo 2 vya uzazi katika wanawake 1,000. Aidha, Ripoti za afya ya uzazi zinaonesha kuwa vifo vingi vya uzazi vinatokea kwa wanawake wazazi wenye umri mdogo kati ya miaka 15 mpaka 18. Kwa hiyo kumpa mtoto wa kike fursa ya elimu inamsaidia yeye kukua kiakili na kimwili na pia kumnusuru na ndoa za utotoni zinazohatarisha maisha yao.

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;** Kwa kuzingatia umuhimu huu, Serikali imekuwa na mipango thabiti ya kuanzisha shule za Sekondari za Kata kwa lengo la kukabiliana na ongezeko kubwa la wanafunzi waliofaulu mtihani wa taifa wa darasa la saba na kukosa nafasi katika shule Kongwe chache zilizokuwepo. Kupitia mpango huu kumekuwa na ongezeko la usajili wa wanafunzi wa kike katika shule za sekondari. Takwimu zinaonesha kuwa Udahili wa wanafunzi wa kike katika shule za sekondari umeongezeka kutoka wanafunzi 728,528 mwaka 2010 hadi wanafunzi 802,554 mwaka 2011 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 74,926 sawa na asilimia 9.2. Hili ni ongezeko kubwa na tunayo kila sababu ya kujivunia.

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana**; Ijapokuwa tumefanikiwa kuongeza idadi ya wasichana wanaojiunga na Sekondari, hali ya unyanyasaji dhidi yao kimwili, kisaikolojia na kiuchumi bado ni changamoto kubwa katika jamii ya kitanzania hasa vijijini. Baadhi ya Wananchi katika jamii yetu bado wanaendeleza Mila zenye madhara kwa kuwatumia Watoto wa Kike kama chombo duni kisicho na msaada wowote katika jamii. Bado kuna jamii ya Watu wanaopenda kuwatumia Watoto wa Kike kwa lengo la kuwaoza, kujipatia mali kwa njia ya mahari na kuwadhalilisha kwa kuwapa mimba na hivyo kuwakatisha masomo. Hili ni jambo la kusikitisha sana!

Takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania ni moja ya nchi zenye kiwango kikubwa cha **mimba za utotoni**, katika kipindi cha miaka minne (4), yaani kuanzia mwaka 2006-2009 jumla ya wanafunzi 16,999 wa Shule za Msingi na Sekondari walikatiza masomo yao kutokana na mimba. Aidha, mdondoko wa wanafunzi wa kike kutokana na utoro umeongezeka kutoka wanafunzi 11,264 mwaka 2009 sawa na asilimia 36.2 hadi wanafunzi 48,026 mwaka 2010 sawa na asilimia

72.7. Hii ni idadi kubwa sana, hali ambayo inaua ndoto zao za kuendelea na masomo na hivyo kuathiri mustakabali wa maisha yao.

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana**; Changamoto hizi na nyingine nyingi zilizopo katika jamii zetu, zimesababisha kuwa na kiwango hafifu cha ufaulu cha wasichana. Katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne uliofanyika 2011, wasichana waliofaulu katika daraja la I-III ni 7% ya wasichana wote na wavulana ni 12%. Hii inatupa picha ni kwa jinsi gani tunatakiwa kuendelea kuwekeza katika elimu ya mtoto wa kike, kwakuwa wengi wao (asilimia 93) wanakosa fursa ya kuendelea na kidato cha tano na hivyo kuathiri maendeleo yao na Taifa letu.

Serikali itaendelea kuchukua hatua kali kwa wote watakaohusika na kuwapa mimba wasichana wa shule. Kwa mujibu wa sheria za nchi ni kosa kwa mwanaume kufanya mapenzi na msichana ambae ana umri wa chini ya miaka 18. Natoa rai kwa jamii kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa pale wanapobaini kuwepo kwa vitendo hivi.

Wizara itaendelea kuwahimiza wasichana kujitunza na kutilia mkazo masomo yao badala ya kujiingiza katika vitendo vya ngono. Wizara pia itaendelea kuwaasa na kuwahimiza wazazi kutimiza majukumu yao katika kuwalea watoto wao kwa kuwajengea maadili mema na pia kufuatilia nyendo zao za kila siku.

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;** Nitumie hadhara hii pia kuongelea suala la **Ukatili Dhidi ya Watoto** kwa kuwa hili lina uhusiano wa karibu zaidi na haki za mtoto wa kike. Mwaka 2009 Serikali kwa kushirikiana na UNICEF, ilifanya utafiti kuangalia hali halisi ya ukatili dhidi ya watoto Tanzania. Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha kuwa kuna kiwango kikubwa cha vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa watoto wa jinsi zote. Hata hivyo, waathirika wakubwa wa ukatili huo ni watoto wa kike walio na umri chini ya

miaka 18. Utafiti huu unaonyesha kuwa watoto watatu (3) wa kike kati ya kumi (10) wamewahi kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kingono kabla hawajatimiza miaka 18. Kwa watoto wa kiume; mtoto mmoja kati ya saba ameshafanyiwa ukatili wa kingono.

Je vitendo hivi ya ukatili vinafanyika wapi? Kwa mujibu wa utatifi huu asilimia 49 ya unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya watoto hufanyika majumbani, wakati asilimia 23 hufanyika njiani wakati wa kwenda au kutoka shule na asilimia 15 ya unyanyasaji hufanyika shuleni.

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;** Takwimu hizi ni za kutisha, Serikali itaendelea kuchukua jitihada za makusudi ili kukomesha aina zote za ukatili dhidi ya watoto. Tutahakikisha sheria zetu zinazowalinda watoto zinakwenda na wakati na kutoa fursa ya haki kutendeka. Tutahakikisha tunatoa elimu ya kutosha kuhusu ukatili dhidi ya watoto hususan watoto wa kike. Tunaamini elimu ni silaha kubwa ya kupambana na uhalifu wa aina yoyote ile.

Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto itaendelea kuelimisha jamii juu ya madhara ya mimba za utotoni kwa jinsi zinavyoathiri maendeleo ya mtoto kisaikolojia, kimwili, kiafya na kuharibu mustakabali mzima wa maisha yao kama wakina mama wa baadae.

Aidha, Wizara yangu itatoa ushirikiano wa kutosha kwa wadau wote watakaoshughulikia tatizo la mimba za utotoni. Leo Katibu Mkuu wa Wizara anashiriki katika uzinduzi wa "Mtandao wa Kukomesha Ndoa za Utotoni Tanzania" katika viwanja ya Mwembeyanga Tandika. Ni imani yangu kuwa Mtandao huu na Kampeni mbalimbali zinazoanzishwa zitachochea jitihada za serikali za kupambana na mimba za Utotoni.

## Uzinduzi wa Kampeni ya "Because I am a Girl"

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;** Baada ya kusema hayo ningependa kutumia fursa hii pia kuzungumzia uzinduzi wa Kampeni ya "Because I am a Girl" - BIAAG inayoendeshwa na shirika la Plan International.

Nimejulishwa kuwa kampeni hii inalenga kuwafikia watoto wa kike takribani milioni nne kote duniani na watoto zaidi ya laki tatu hapa kwetu Tanzania. Lengo lake ni kutokomeza ukatili wa kijinsia, kutetea haki za watoto wa kike ili kuwaondoa katika wimbi la umaskini. Nimefarika kusikia kuwa kampeni hii imejikita katika kufanya ushawishi katika ngazi mbalimbali katika jamii ili kutokomeza mazingira magumu ya unyanyasaji yanayomkabili mtoto wa kike katika familia, shule na jamii kwa ujumla.

**Wageni waalikwa, mabibi na mabwana;** Nitumie fursa hii kutoa shukurani kwa uongozi wa Plan Internationalwa kushirikisha Serikali katika kampeni hii. Sisi Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto tutatoa ushirikiano mkubwa kuhakikisha kuwa kampeni hii inafanikiwa. Nimetaarifiwa kuwa Kampeni hii itahusisha mikakati ya kuelimisha jamii, kuwapa wasichana ujuzi, elimu ya kujitambua, kujiamini na kushiriki kikamilifu katika masuala ya maendeleo yao na ulinzi katika ngazi ya familia, jamii, wilaya na Taifa. Muhimu pia ni kuwa kampeni hii haitambagua mtoto wa kiume kwa sababu ana mchango mkubwa katika kuhakikisha watoto wa kike wanapata haki zao. Pia wataguswa na fursa ambazo zitakuwa zimeelekezwa kwa watoto wa kike. Ili kuifanya kampeni hii kuwa endelevu, ninawahimiza kuwatumia maafisa maendeleo ya jamii ambao wapo katika kila Halmashauri na katika baadhi ya kata katika shughuli mbalimbali mtakazozitekeleza.

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;** Nimefarijika kusikia kuwa sambamba na uzinduzi huu shirika la Plan limekuwa likijihusisha na haki za mtoto wa kike kwa kupitia kampeni ya "Jifunze bila woga" (Learn Without Fear). Na hii imewezesha kujengwa kwa Mabweni ya wasichana katika shule za sekondari Sangara (Ilala); Buhongwa (Ilemela – Mwanza); Ihanamilo (Geita). Mabweni haya yote yameweza kutosheleza idadi ya wanafunzi wa kike 300 pamoja na huduma bora za maji, vyoo na umeme/sola. Pia kupitia mradi wa kuwasaidia wasichana kielimu shirika la Plan limeweza kuwafikia wasichana 250 katika wilaya ya kilombero.

Binafsi na Wizara yangu ya Maendeleo ya Jamii , Jinsia na watoto, tunafarijika na kampeni hii kwa kuwa ni hatua sahihi ya kimkakati ya kumwezesha mtoto wa kike kutimiza ndoto yake kielimu lakini pia inachangia uwiano wa kijinsia kwa ajili ya maendeleo ya jamii nzima. Kipekee niwapongeze Uongozi mzima wa Shirika la Plan International kwa jitihada kubwa mliyofanya katika kuwezesha ujenzi wa mabweni. Hii inauthibitishia umma wa watanzania dhamira mliyonayo ya kuhakikisha kuwa elimu kwa mtoto wa kike inapewa kipaumbele.

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;** Kwa kuhitimisha napenda kuwakumbusha kuwa Jukumu la kuwalinda watoto ni la kila mmoja wetu. Tutambue kwamba hakuna mtu mmoja au taasisi yenye ujuzi, maarifa na rasilimali za kutosha kukidhi mahitaji yote ya kumlinda mtoto. Kwa hiyo natoa wito kwa wadau wote wa maendeleo ya Mtoto kuunga mkono jitihada zilizoanzishwa na wenzetu wa Plan International katika kuwalinda watoto wa kike dhidi ya ukatili na unyanyasaji.

Pia kwa ndugu zetu **viongozi wa dini,** na viongozi katika ngazi ya jamii, mtumie fursa mnazokuwa nazo na waumini pamoja na wananchi katika kufikisha ujumbe huu wa kuwalinda na kuwapatia watoto wa kike haki zao.

Kwenu **wazazi na walezi**, ninyi ni watu muhimu sana katika suala hili,, mnatakiwa kutambua na kutekeleza wajibu wenu katika kuwalea watoto kwa kuwapatia fursa sawa bila kuwabagua.

Na kwa **watoto wetu wapendwa**, mtambue kwamba mna haki ya kupata fursa sawa katika familia na jamii kwa ujumla kwa maendeleo yenu, lakini pia mna wajibu mkubwa wa kuzitumia fursa ipasavyo na kujilinda kwa kufuata maadili mazuri mnayopata kwa wazazi, walezi na jamii.

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana**; Baada ya kusema hayo kwa mara nyingine tena napenda niwashukuru kwa kunialika kuwa Mgeni rasmi katika sherehe hizi na kuwatakia kila la Kheri katika Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike kwa mwaka 2012. Na ninapenda sasa kutamka rasmi kuwa Kampeni ya "Because I am a Girl" imezinduliwa rasmi.

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA.**